**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO KILICHOKETI TAREHE 25/10/2021 KATIKA UKUMBI WA KITUO CHA KILIMO LAELA**

**Kumb. SDC/FAP-05/10/2021-2022**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Mhe. Kalolo Gerald Ntilla | - Diwani Kata ya Muze | - | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Apolinary Macheta | - Diwani Kata ya Milepa | - | Mjumbe |
| 3. Mhe. Norasco F. Kafolah | - Diwani Kata ya Mpui | - | Mjumbe |
| 4. Mhe. Patrick O. Mbalalile | - Diwani Kata ya Mfinga | - | Mjumbe |
| 5. Mhe. Credo Petro Mshindo | - Diwani Kata ya Mwadui | - | Mjumbe |
| 6. Mhe. Abel Msumbachika | - Diwani Kata ya Mpwapwa | - | Mjumbe |
| 7. Mhe. Ludovick D. Akilimali | - Diwani Kata ya Kilangawana | - | Mjumbe |
| 8. Mhe. Paulina Kisiwa | - Diwani Viti Maalum Tarafa ya Mtowisa | - | Mjumbe |
| 9. Mhe. Claudia Kanzala | - Diwani Viti Maalum Tarafa ya Kipeta | - | Mjumbe |
| 10. Mhe. Omelina Mgawe | - Diwani Viti Maalum Tarafa ya Laela | - | Mjumbe |
| 11. Mhe. Kazonda G. Daimond | - Diwani Kata ya Mnokola | - | Mjumbe |
| 12. Mhe. Deus C. Sangu | - Mbunge Jimbo la Kwela | - | Mjumbe |
| 13. Mhe. Bupe V. Mwakang'ata | - Mbunge V/Maalum Jimbo la Kwela | - | Mjumbe |

**WATAALAM WALIOHUDHURIA.**

1. Bi. Lightness S. Msemo - Mkurugenzi Mtendaji (W)
2. Bw. Hamis Mkelle - Afisa Utawala na Utumishi (W)
3. Bw. Linus Sikainda - Kaimu Afisa Mipango (W).
4. Bi. Dorah Sospeter - Kaimu Afisa Manunuzi (W)
5. Bw. Peter Mollel - Mweka Hazina (W)
6. Bw. Leonard Mwandendi - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)
7. Bw. Joseph Millinga - Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
8. Bw. Benedicto Silla - Kaimu Afisa TEHAMA (W)
9. Bi. Jojina Nyamboko - Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W)
10. Bi. Fanisia Malesa - Kaimu Mratibu wa UKIMWI (W)
11. Bw. Anderson Mwakyembe - Afisa Usafirishaji (W)
12. Bw. Ambwene Yonah - Afisa Habari
13. Bi. Bahati Mgimwa - Afisa Uchaguzi (W)
14. Bw. Juma Mseya - Kaimu Afisa Ufugaji Nyuki (W)
15. Bw. Marius Kapufi - Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
16. Bi. Veronica Mwandiga - Afisa Biashara (W)
17. Bi. Happyness Amlima - Kaimu Afisa Sheria (W)
18. Bw. Filbert Msemwa - Kaimu Afisa Ardhi na Mazingira (W)
19. Bw. Godfrey Zuberi - Afisa Ardhi Msaidizi
20. Dkt. Nicodemus Masosota - Kaimu Mganga Mkuu (W)
21. Bw. Sigfrid Mapunda - Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W)
22. Bw. Kabura James Philip - Kaimu Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W)
23. Bw. Ipyana Mwakubali - Afisa Mapato (W)



CamScanner

## WATAALAM WASIOHUDHURIA.

1. Bw. Godfrey Maufi - Kaimu Afisa Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu (W)
2. Bi. Fanikio I. Bitende - Afisa Elimu Sekondari (W)
3. Bw. Chande A. Juma - Afisa Ardhi na Maliasili (W)
4. Bw. Dennis Maghala - Afisa Mifugo na Uvuvi (W) - Kwa Taarifa
5. Bi. Patricia J. Mpewa - Kaimu Afisa Elimu Msingi (W) - Kwa Taarifa
6. Bw. Herbert Mbise - Afisa Sheria (W) - Kwa Taarifa

## SEKRETARIETI:

1. Louis Kinyonto - Katibu wa Kamati (W)
2. Bw. Aloyce Pius Mwingo - Katibu wa Kamati

## MUHTASI NA. SDC/FAP-03/01/10/2021-2022: KUFUNGUA KIKAO.

Kabla ya kufungua Kikao Katibu wa kikao aliwakaribisha Wajumbe katika kikao na kisha alimkaribisha Mwenyekiti wa kikao ili aweze kufungua kikao. Mwenyekiti alifungua Kikao mnamo saa 07:56 mchana.

## MUHTASI NA. SDC/FAP-05/02/10/2021-2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO.

Agenda zifuatazo zilisomwa na kuthibitishwa kuwa agenda za Kikao;-

1. Kufungua Kikao.
2. Kusoma na kuthibitisha agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Kikao cha tarehe 12/09/2021.
4. Taarifa ya utekelezaji wa yatokanayo na;-
   I. Kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango tarehe 12/09/2021.
   II. Kikao cha Baraza la Madiwani kilichoketi tarehe 21/08/2021.
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Septemba 2021.
6. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022.
7. Taarifa ya Mkaguzi wa Ndani katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022.
8. Taarifa ya uhakiki wa fedha za makusanyo ndani zilizotumika nje ya mfumo.
9. Taarifa ya Manunuzi katika kipindi cha mwezi Septemba 2021.
10. Taarifa mbalimbali:-
    I. Taarifa ya kesi za Halmashauri.
    II. Taarifa ya zoezi la usajili wa vitambulisho vya Wajasiriamali na Watoa Huduma wadogo.
    III. Taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji inayojengwa Makao Makuu ya Halmashauri Laela.
    IV. Maendeleo ya ujenzi wa Wodi tatu katika Hospitali ya Wilaya Mtowisa.



CamScanner

11. Mapendekezo ya kuajiri madereva wawili wa mkataba.
12. Mapendekezo ya uendelezaji wa stendi ya mabasi Laela.
13. Ombi la kuidhinishiwa matumizi ya tshs 28,350,000/= kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi ya maendeleo.
14. Mapendekezo ya utekelezaji wa miradi.
15. Mpango kazi na rejista ya kazi za kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
16. Maombi ya kubadili matumizi ya fedha shs 10,000,000/= kutoka chanjo ya mifugo kwenda ukarabati wa machijio Laela.
17. Maombi ya mkopo wa fedha shs 47,750, 000/=kutoka wizara ya ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi kwa ajili ya miradi ya kutwa, kupanga, kupima na kukamilisha upangaji wa mji wa Laela.
18. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.
19. Kufunga Kikao.

**MUHTASI NA. SDC/FAP-05/03/10/2021-2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 12/09/2021.**

Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 12/09/2021 ulisomwa na kusainiwa mara baada ya kufanyiwa marekebisho katika baadhi ya maeneo.

**MUHTASI NA. SDC/FAP-03/04/10/2021-2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO**

Iliwasilishwa taarifa ya utekelezaji wa yatokanayo na Kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kilichoketi tarehe 12/09/2021 na mara baada ya kuwasilishwa, Wajumbe waliipitia na yafuatayo yalijitokeza;-

**Suala la matengenezo ya magari.**

Katika kujadili suala hili ilielezwa kuwa, Kwa kuwa Menejimenti imekamilisha matengenezo ya magari matano, taarifa ya matengenezo hayo ilitakiwa kuwasilishwa katika kikao ili Wajumbe waipitie taarifa hiyo, baada ya kutolewa hoja hii, Wajumbe waliazimia kuwa;-

**Azimio:**

Kutokana na Menejimenti ya Halmashauri kukamilisha matengenezo ya magari matano, taarifa ya gharama za matengenezo ya magari hayo ziwasilishwe katika kikao kijacho.

**Ufuatiliaji wa mgogoro wa ununuzi wa jenereta.**

Katika kujadili suala hili, Wajumbe waliazimia kuwa;-



CamScanner

**Azimio:**

Kutokana na Menejimenti ya Halmashauri kuendelea kufanya ufuatiliaji wa taarifa za ununuzi wa jenereta, katika kikao kijacho iwasilishwe taarifa ya mchakato wa ununuzi wa jenereta hiyo.

**Suala la kujibu hoja za Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa na hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

Katika kujadili jibu la utekelezaji juu ya majibu ya Hoja za Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa na hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Wajumbe walieleza kuwa Menejimenti ya Halmashauri inatakiwa kuhakikisha kuwa hoja zote zinapatiwa majibu na kuwasilishwa kwa Mkaguzi Mkazi ili ziweze kufungwa, baada ya kutolewa hoja hiyo wajumbe waliazimia kuwa;-

**Azimio**

Baada ya kutolewa hoja hiyo Wajumbe waliazimia kuwa;-

**Azimio:-**

Kutokana na kutokamilika kwa kazi ya kujibu hoja za Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa na hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Menejimenti ya Halmashauri iendelee kuzifanyia kazi hoja hizo ili ziweze kuhakikiwa na kufungwa.

**Suala la uanzishaji wa stendi katika Mji Mdogo wa Kilyamatundu na Muze.**

Baada ya kupitia majibu yaliyowasilishwa na Menejimenti ya Halmashauri juu ya uanzishaji wa stendi katika Mji mdogo wa Muze na Kilyamatundu, Wajumbe waliazimia kuwa;-

1. Kutokana na eneo la ujenzi wa stendi katika Kijiji cha Muze kufanyiwa uthamini na uthamini huo kuwa na gharama ambayo Halmashauri inaweza kufidia, Menejimenti ya Halmashauri ilipe fidia hiyo ili ujenzi wa Stendi hiyo uanze mara moja.
2. Kutokana na eneo la ujenzi wa stendi katika Mji Mdogo wa Kilyamatundu kuwa na fidia kubwa, Menejimenti ya Halmashauri ione uwezekano wa kufidia eneo ambalo halina makazi ya watu ili stendi hiyo ianze kujengwa.

**Suala la usimamizi wa msitu wa Ilemba**

Katika kujadili suala hili, Wajumbe walieleza kuwa, kwa sasa kuna uharibifu mkubwa wa msitu wa Ilemba na hivyo inahitajika juhudi ya haraka ili kuzuia uharibifu wa msitu huo, baada ya kutolewa maelezo hayo, Wajumbe waliazimia kuwa;-

**Azimio**

Kutokana na uharibifu wa msitu wa Ilemba unaoendelea, Menejimenti ya Halmashauri ichukue juhudi za haraka kufanya doria kwa ajili ya kudhibiti watu wote waliovamia msitu huo.



CamScanner

**...a la ukarabati wa choo katika mnada wa mifugo Kilyamatundu**

...atika kujadili jibu la utekelezaji wa agizo hili, Wajumbe walieleza kuwa, kutokana na hali ya uchakavu wa choo katika mnada wa mifugo kilyamatundu, Menejimenti ya Halmashauri inatakiwa kuhakikisha kuwa choo hiyo inafanyiwa ukarabati mara moja. Baada ya kutolewa maelezo hayo, Wajumbe waliazimia kuwa;-

**Azimio**

Kutokana na uchakavu wa choo katika mnada wa mifugo Kilyamatundu na kutofanyika kwa ukarabati wa choo hicho kwa muda mrefu, Menejimenti ya Halmashauri ihakikishe inafanya ukarabati wa choo hicho mara moja.

**Suala la usimamizi wa vibarua wa magetini**

Katika kujadili suala hili, Wajumbe walieleza kuwa wapo vibarua walioajiriwa katika kazi ya ukusanyaji wa mapato na hawatekelezi majukumu yao ipasavyo jambo ambalo linapelekea kupotea kwa mapato ya Halmashauri. Kutokana na hali hiyo, Wajumbe waliazimia kuwa;-

**Azimio**

Kutokana na taarifa za utendaji kazi usiofaa wa baadhi ya vibarua wa mikataba waliopatiwa kazi ya kukusanya mapato, Menejimenti ya Halmashauri ifanye ufuatiliaji wa suala hii na ikibainika kuwa wapo vibarua walio na utendaji kazi usiofaa, waondolewe katika nafasi hizo na vibarua wengine waajiriwe.

**MUHTASI NA. SDC/FAP-05/05/10/2021-2022: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KATIKA KIPINDI CHA MWEZI JULAI 2021 HADI SEPTEMBA , 2021.**

Iliwasilishwa taarifa ya mapato na matumizi katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Septemba, 2021 kama ifuatavyo;-

**MAPATO.**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2021/2022, Halmashauri ilikisia kukusanya jumla ya shilingi 40,424,734,297/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,760,500,000/= ni makisio ya mapato kutoka katika vyanzo vya ndani, shilingi 1,881,153,380/= ni makisio ya mapato ya fedha za matumizi mengineyo (OC) na fedha za ruzuku ya fidia ya kodi (OC-GPG), shilingi 25,015,906,917/= ni makisio ya mapato ya fedha za mishahara ya Watumishi na shilingi 10,761,173,999.97/= ni makisio ya mapato ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka Serikali Kuu na Wahisani.

Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Septemba 2021, Halmashauri imepokea na kukusanya jumla ya shilingi 6,751,698,717/= kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwa ni sawa na 17% ya lengo la mwaka 2021/2022. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama ifuatavyo;-



CamScanner

**...ato maeneo yasiyopata ruzuku (Vyanzo vya Ndani).**

...atika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Septemba 2021, Halmashauri imeweza kukusanya ...umla ya shilingi 781,688,987.30 sawa na 28% ya lengo la mwaka la shilingi 2,760,500,000/=. (Mchanganuo wa mapato ya fedha hizo uliambatanishwa katika taarifa).

**Mapato maeneo yanayopata ruzuku (Mishahara, OC na OC – GPG).**

Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Septemba 2021, Halmashauri imepokea jumla ya shilingi 5,404,599,249.98. Kati ya fedha hizo, mishahara ya Watumishi ni shilingi 4,987,053,000/= sawa na 20% na shilingi 417,546,249.98 ni fedha za matumizi mengineyo (OC) na fedha za ruzuku ya fidia ya kodi (OC-GPG), sawa na 22%.

**Mapato ya fedha za miradi ya maendeleo.**

Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo, katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Septemba 2021, Halmashauri imepokea fedha kiasi cha shilingi 565,410,479.28 sawa na 5%.

**MATUMIZI:-**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2021/2022, Halmashauri ilikisia kutumia jumla ya shilingi 40,424,734,297/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,760,500,000/= ni makisio ya matumizi ya fedha za makusanyo yatokanayo na vyanzo vya ndani, shilingi 1,881,153,380/= ni makisio ya matumizi ya fedha za matumizi mengineyo (OC) na fedha za ruzuku ya fidia ya kodi (OC-GPG), shilingi 25,015,906,917/= ni makisio ya matumizi ya fedha za mishahara ya Watumishi na shilingi 10,761,173,999.97/= ni makisio ya matumizi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Septemba 2021, Halmashauri imetumia jumla ya shilingi 5,771,937,959/= kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwa ni sawa na 14% ya lengo la mwaka 2021/2022. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama ifuatavyo;-

**Matumizi maeneo yasiyopata ruzuku (Vyanzo vya Ndani).**

Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Septemba 2021, Halmashauri imetumia jumla ya shilingi 531,691,259/= sawa na 19% ya lengo la mwaka la shilingi 2,760,500,000/=. (Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo uliambatanishwa katika taarifa).

**Matumizi maeneo yanayopata ruzuku (Mishahara, OC na OC – GPG).**

Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Septemba 2021, Halmashauri imetumia jumla ya shilingi 5,233,766,700/=. Kati ya fedha hizo, mishahara ya Watumishi ni shilingi 4,987,053,000/= sawa na 20% na shilingi 246,713,700/= ni fedha za matumizi mengineyo (OC) na fedha za ruzuku ya fidia ya kodi (OC-GPG), sawa na 13%.



CamScanner

## ...umizi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo.

Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo, katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Septemba 2021, Halmashauri imetumia fedha kiasi cha shilingi 6,480,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Matumizi ya fedha za Miradi ya Maendeleo zilizovuka mwaka**

Wakati tunafunga mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ilisalia na fedha kiasi cha shilingi 1,544,525,590/= kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Septemba, 2021 kiasi cha shilingi 207,100,406.12 kimetumika na kubaki shilingi 1,337,425,183.88; Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo ni kama ifuatavyo;-

| NA. | JINA LA MRADI | KIASI KILICHOVUKA MWAKA | KIASI KILICHOLIPWA | SALIO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi | 921,504,470/= | 86,959,114/= | 834,545,356/= |
| 2. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya | 437,021,120/= | 39,141,292.12 | 397,879,527.88 |
| 3. | Ujenzi wa Zahanati | 105,000,000/= | 81,000,000/= | 24,000,000/= |
| 4. | Ujenzi wa vyoo vya SWASH - Afya | 81,000,000/= | - | 81,000,000/= |
| | **JUMLA** | **1,544,525,590/=** | **207,100,406.12** | **1,337,425,183.88.** |

Pamoja na taarifa hiyo iliambatanishwa taarifa ya madeni ya wakusanyaji mapato (defaulters) ikionesha kuwa, Halmashauri imefanya ufuatiliaji wa madeni ya wakusanyaji (defaulters) na kufanikiwa kupata kiasi cha shilingi 11,179,500/= kutoka kwa wadaiwa wa muda mrefu, na kiasi cha shilingi 80,586,500/= kutoka kwa wadaiwa wapya. Hivyo, jumla ya fedha zilizokusanywa ni shilingi 91,766,000/=. Mchanganuo wa madeni hayo uliambatishwa katika taarifa.

Pamoja na taarifa hiyo iliambatishwa mikakati ya kuhakikisha makusanyo yanafanikiwa na kuvuka malengo.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Wajumbe waliijadili na yafuatayo yalijitokeza;-

**Suala la uboreshaji wa ukusanyaji wa mapato katika Kata ya Mnokola.**

Katika kujadili suala la namna ya kuongeza mapato, ilielezwa kuwa Kata ya Mnokola ina mashine moja ya kukusanyia mapato. Ili kuweza kuongeza ukusanyaji wa mapato katika Kata hiyo, mashine moja inatakiwa kuongezwa kwa ajili ya kukusanyia mapato katika Kijiji cha Mititi. Baada ya kutolewa hoja hiyo, Wajumbe waliazimia kuwa;-

**Azimio**

Ili kuboresha ukusanyaji wa mapato katika Kata ya Mnokola, Menejimenti ya Halmashauri ihakikishe mashine moja ya kukusanyia mapato inaongezwa katika Kata hiyo.



CamScanner

...a la ukusanyaji wa ushuru wa mazao yanayouzwa NFRA

...wasishwa taarifa kuwa, Wafanyabiashara wanaosafirisha mazao kwenda kuuza kwa Wakala ...a Taifa wa Chakula (NFRA) wamekuwa wakikwepa kulipa ushuru wa wazao na hivyo kupelekea Halmashauri kukosa mapato. Kutokana na hali hiyo Wajumbe waliazimia kuwa;-

**Azimio**

Kutokana na kutokutozwa kwa ushuru wa mazao yanayosafirishwa na kuuzwa NFRA, Menejimenti ya Halmashauri iwaagize Watendaji wa Kata na Vijiji wahakikishe kila mazao yanayosafirishwa kwenda NFRA yanalipiwa ushuru.

**MUHTASI NA. SDC/FAP-05/06/10/2021-2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA YA MWAKA 2021/2022.**

Iliwasilishwa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikionesha kuwa, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri iliidhinishiwa kupokea na kutumia fedha kiasi cha shilingi 12,426,554,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Septemba 2021, Halmashauri imepokea kiasi cha shilingi 950,313,489/= sawa na 7.6% za fedha za miradi. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi 567,563,383/= ni mapokezi ya fedha nje ya ukomo wa bajeti.

Kwa upande wa Matumizi, katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Septemba 2021 fedha zilizotumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni shilingi 239,801,600.29/= sawa na 42.25% ya fedha zilizopokelewa. Mchanganuo wa mapokezi na matumizi ya fedha hizo uliambatanishwa katika taarifa.

Baada ya kuwasilishwa taarifa hiyo, Wajumbe waliipokea na kuiridhia.

**MUHTASI NA. SDC/FAP-05/07/10/2021-2022: TAARIFA YA UKAGUZI WA NDANI KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA YA MWAKA 2021/2022.**

Iliwasilishwa taarifa ya Ukaguzi wa Ndani wa Hesabu za Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022 ikionesha hoja zilizoibuliwa na Mkaguzi wa Ndani na mara baada ya kuwasilishwa, Wajumbe walizipitia hoja zote zilizoibuliwa na kuazimia kuwa;-

**Azimio:**

Menejimenti ya Halmashauri ihakikishe kuwa hoja zote zilizojitokeza katika taarifa ya Mkaguzi wa Ndani katika pindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022 zinafanyiwa kazi na kufungwa na ikiwa hoja hizo hazitofanyiwa kazi wahusika waliosababisha hoja wachukuliwe hatua za kinidhamu.



CamScanner

## MUHTASI NA. SDC/FAP-05/08/10/2021-2022: TAARIFA YA UHAKIKI WA FEDHA ZA MAKUSANYO YA MAPATO ZILIZOTUMIKA NJE YA MFUMO (DEFAULTERS).

Iliwasilishwa taarifa kuwa, Kitengo cha ukaguzi wa Ndani kimekamilisha uhakiki wa nyaraka za matumizi ya fedha nje ya mfumo kwa Maafisa Watendaji wa Kata ili ziweze kulipwa na kupelekwa Benki. Sababu ya uhakiki huo ni kutokana na Watendaji wa Kata kutumia fedha nje ya Mfumo kwa idhini ya Afisa Masuhuli na kupelekea kuwepo kwa Wadaiwa wa muda mrefu katika Mfumo wa mapato.

Taarifa hiyo ilieleza zaidi kuwa, suala hili lilipopelekwa katika mamlaka zingine iliamriwa madeni hayo yalipwe ili kujua kiasi halisi cha fedha anachodaiwa Mtendaji baada ya malipo ya fedha hizo kufanyika.

Matokeo ya uhakiki huo hadi kuishia Mei 2021 ni kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini;-

MCHANGANUO WA UHAKIKI WA MATUMIZI

| MATUMIZI YALIYOWASILISHWA | MATUMIZI YALIYOKATALIWA | MATUMIZI YALIYOKUBALIWA |
|---|---|---|
| 90,094,500 | 55,026,000 | 35,068,500 |

Baada ya kuwasilishwa taarifa hiyo, Wajumbe waliijadili na kuazimia kuwa;-

**Azimio**

1. Kutokana na uhakiki wa fedha zilizokusanywa na kutumiwa kabla ya kuwasilishwa Halmashauri, Watumishi wote ambao hawakuwasilisha fedha watakiwe kuwasilisha fedha na watakaoshindwa hatua stahiki zichukuliwe dhidi yao.
2. Kutokana na uwepo wa fedha zilizochukuliwa na Menejimenti ya Halmashauri kwa matumizi mbalimbali na kuridhiwa baada ya Ukaguzi, fedha hizo ziondolewa katika mfumo wa mapato ili zisisomeke kama deni.

## MUHTASI NA. SDC/FAP-05/09/10/2021-2022: TAARIFA YA MANUNUZI KATIKA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2021.

Iliwasilishwa taarifa ya manunuzi katika kipindi cha mwezi Septemba 2021 ikionesha kuwa, fedha zilizotumika kwa ajili ya manunuzi ni shilingi 108,151,108.61 kwa mchanganuo ufuatao;-

| | | |
|---|---|---|
| 1. Idara ya Utawala na Utumishi | - | 76,593,008.61 |
| 2. Idara ya Afya | - | 4,037,400/= |
| 3. Idara ya Fedha | - | 2,459,300/= |
| 4. Kitengo cha TASAF | - | 25,061,400/= |
| **Jumla Kuu** | - | **108,151,108.61** |

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Wajumbe waliipitia na kuiridhia.



CamScanner

**...HTASI NA. SDC/FAP-05/10/10/2021-2022: TAARIFA MBALIMBALI;-**

**I. TAARIFA YA KESI MBALIMBALI ZA HALMASHAURI HADI KUFIKIA SEPTEMBA, 2021.**

Iliwasilishwa taarifa ikionesha kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2021 Halmashauri ilikuwa na kesi saba ambazo zipo katika hatua mbalimbali kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo;-

| NA. | NAMBA YA KESI | WADAAWA | MADAI | MAHAKAMA | HATUA | KIWANGO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Application no 8/2017 | JALEMA Co Ltd Vs.<br>1. Giah Emmanuel Sayi<br>2. Sumbawanga Distict Council<br>3. TanzaniaPosta l Bank | Madai ya fedha za kandarasi ya ujenzi zilizolipwa kwenye akaunti ambayo haiko kwenye Mkataba na Halmashauri | Mahakama ya Wilaya | Kusikilizwa | 44,473,232/= |
| 2. | Application No 8/2018 | Bies Melimeli Vs Serikali ya Kijiji cha Mumba | Mgogoro wa umiliki wa Ardhi kati ya Bies Melimeli na Serikali ya Kijiji cha Mumba | Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya Sumbawanga | Kusikilizwa | |
| 3 | Application no 7/2021 | Adosta Investment Co ltd Vs. Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga | Utekelezaji wa hukumu iliyotokana na kesi ya Madai namba 8 of 2016. | Mahakama ya Wilaya | Kusikilizwa | 268,546,265.60 |
| 4 | Misc Land Appl No 73/2021 | Paulo Wazimila Kipeta vs Serikali ya Kijiji cha Mtowisa B | Maombi ya marejeo baada ya uamuzi wa Baraza la Kata la Mtowisa | Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya Sumbawanga | Kusikilizwa | |
| 5 | Land Appl No 42/2020 | Yuda Kalulu & Another Vs Serikali ya Kijiji cha Mkunda | mgogoro wa umiliki wa ardhi kati ya yuda kalulu na serikali ya kijiji cha mkunda. | Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya Sumbawanga | Kusikilizwa | |
| 6 | Misc Land Appl.No 61/2020 | Yunge Nkuba vs Serikali ya Kijiji cha Talanda | Maombi ya marejeo baada ya uamuzi wa Baraza la Kata | Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya Sumbawanga | Kusikilizwa | |
| 7 | Misc Land Appl No 62/2020 | Tumaini Lusambana vs Serikali ya Kijiji cha Talanda | Maombi ya marejeo baada ya uamuzi wa Baraza la Kata | Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya Sumbawanga | Kusikilizwa | |

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Wajumbe waliipokea na kuiridhia.



CamScanner

## II. TAARIFA YA ZOEZI LA USAJILI WA VITAMBULISHO VYA WAJASILIAMALI NA WATOA HUDUMA WADOGO.

Iliwasilishwa taarifa kuwa, zoezi la usajilli wa Wafanyabiashara na Watoa huduma wadogo walio katika Halmashauri yetu linaendelea kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini;-

| Walioomba vitambulisho | Maombi yaliyolipiwa | Vitambulisho vilivyochapishwa | Vitambulisho vilivyofika kwa Mkurugenzi | Jumla ya fedha iliyokusanywa |
|---|---|---|---|---|
| 345 | 260 | 240 | 195 | 5,200,000/= |

Vitambulisho vilivyopokelewa vimegawiwa kwa wahusika kupitia Watendaji wa Kata na Vijiji. Aidha, katika kuendesha zoezi hilo zipo changamoto mbalimbali ikiwemo wafanyabiashara wengi kutokuwa na simu janja na wengine kushindwa kuzitumia katika kufanya usajili, baadhi ya wafanyabiashara kutokuwa na namba za NIDA, pamoja na kuchelewa kufika kwa vitambulisho vilivyolipiwa.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Wajumbe waliipokea na kuiridhia.

## III. TAARIFA YA MAENDELEO YA UJENZI WA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI INAYOJENGWA MAKAO MAKUU YA HALMASHAURI LAELA.

Iliwasilishwa taarifa kuwa, Halmashauri imepokea shs 1,000,000,000/= kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri Makao Makuu katika Mji Mdogo wa Laela. Mradi huo ulianza utekelezaji wake mwezi Mei 2021 na unatarajiwa kukamilika Mwezi Desemba 2021. Mradi huo unatekelezwa kwa kutumia njia ya 'Force Account' na unatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi 2,738,017,700/=

Hadi sasa kiasi cha fedha kilichotumika ni shilingi 169,637,703/= na hivyo kubaki na shilingi 830,362,297/=. Kazi zilizofanyika hadi sasa ni pamoja na utafiti wa udongo, usafishaji wa eneo, ujenzi wa uzio, uchimbaji wa Msingi, kusuka nondo na ujenzi wa chumba cha kuhifadhia vifaa vya ujenzi. Mchanganuo zaidi wa shughuli zilizotekelezwa uliambatishwa katika taarifa.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Wajumbe waliipitia na kuiridhia.

## IV. MAENDELEO YA UJENZI WA WODI TATU KATIKA HOSPITALI YA WILAYA MTOWISA.

Iliwasilishwa taarifa kuwa, Halmashauri ilianza kutekeleza kazi ya ujenzi wa wodi tatu katika Hospitali ya Wilaya na hadi kufikia tarehe 24/10/2021 ujenzi wa jengo hilo ulikuwa katika hatua ya msingi na kazi ilikuwa imesimama kutokana na kutolipwa kwa fedha za mafundi na vifaa kwa ajili ya uendelezaji wa mradi.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Wajumbe waliipokea na kuiridhia.



CamScanner

**[illegible]TASI NA. SDC/FAP-05/10/11/2021-2022: MAPENDEKEZO YA KUAJIRI MADEREVA [illegible] WA MKATABA.**

[illegible]wasilishwa taarifa kuwa, Halmashauri inakabiliwa na uhaba mkubwa wa madereva ambapo [illegible]mbapo kwa sasa Menejimenti inaomba kuajiri madereva nane ili kuweza kukabiliana na uhaba [illegible]huo. Baada ya kuwasilishwa taarifa hiyo, Wajumbe waliipokea na kuiridhia pendekezo ya kuajiri madereva nane kwa mkataba.

**MUHTASI NA. SDC/FAP-05/12/10/2021-2022: MAPENDEKEZO YA UENDELEZAJI WA STENDI YA MABASI LAELA.**

Iliwasilishwa taarifa ya mapendekezo ya uendelezaji wa stendi ya mabasi Laela juu ya mambo makuu yafuatayo;-

**1. Mabadiliko ya viwango vya malipo ya vibanda vya wajasiriamali stendi ya laela**

Katika suala hili ilielezwa kuwa, kasi ya uchukuaji na urejeshaji wa mikataba iliyojazwa hairidhishi kwani hadi sasa ni wajasiriamali 8 tu waliochukua mikataba lakini hakuna hata mmoja aliyerejesha mkataba licha ya kuwa tangazo liliwataka kurejesha mikataba iliyojazwa na kusainiwa tarehe 16/09/2021.

Miongoni mwa sababu zilizoliathiri zoezi la uchukuaji na urejeshaji wa mikataba ni pamoja na;-

i. Kubadilika kwa muda wa ukamilishaji wa ujenzi wa vibanda kutoka miezi 6 hadi miezi 3, kinyume na tangazo la awali.
ii. Kiwango cha kodi ya pango cha shilingi 40,000/= kwa mwezi kimeonekana kuwa kikubwa kwa sababu walizosema kuwa eneo hilo bado haliko vizuri katika biashara.
iii. Malipo ya pango ya shilingi 20,000/= kila mwezi baada ya kukamilisha ni makubwa, hivyo waliomba ipunguzwe.

Kutokana na hali hiyo Kamati ya uendelezaji wa Stendi ilipendekeza mambo yafuatayo;-

i. Muda wa ujenzi wa kibanda ubaki miezi 6 badala ya 3.
ii. Kiwango cha kodi ya pango kibaki kuwa shilingi 40,000/= ambapo mpangaji atatakiwa kulipa 10,000/= tofauti na 20,000/= ilivyokuwa awali kwa mwezi mpaka pale atakapokuwa amemaliza kurejesha gharama zake za ujenzi, kwa uwiano wa 75% kwa 25% badala ya 50% kwa 50%.
iii. Kwa kuwa kumekuwa na kusuasua kwa zoezi la uchukuaji na urejeshaji wa mikataba, mjenzi mwenye nia ya kujenga ndiye apewe kipaumbele kujenga badala ya kutoa namba za vibanda.
iv. Waombaji wote walioshinda nafasi za kujenga vibanda vya biashara wapewe taarifa ya kushiriki kikao kwa ajili ya kupewa taarifa ya maboresho ya mkataba.



CamScanner

**Hali ya miundombinu kuelekea msimu wa masika**

Kutokana na hali ya ardhi ya eneo la stendi, Kamati ya uendelezaji wa Stendi inapendekeza kuwe na maboresho ya Msingi ya miundombinu yanayotakiwa kufanyika ili stendi iweze kuendelea kutoa huduma hata wakati wa msimu wa masika. Maboresho hayo ya miundombinu ni pamoja na;-

i. Kuimarisha eneo lote la kuingilia, kutokea magari (Drive way) na kupaki magari kwa kuweka kifusi cha changarawe (Grade One) kitakachohimili hali ya masika
ii. Ijengwe mifereji eneo la juu na pembeni ya stendi ili kudhibiti maji yasiharibu eneo la ndani ya stendi.
iii. Njia za kuelekea chooni ziwekwe kifusi na kushindiliwa,

Kazi hizi zote zinakadiriwa kuwa na gharama ya shilingi 74,000,000/=.

iv. Kuongeza shimo la pili la kupokelea maji ya choo ambalo linakadiriwa kugharimu shilingi 2,497,000/=

Hivyo, gharama nzima ya uimarishaji wa stendi inakuwa shilingi 76,497,000/=. Kwa kuwa kiasi kilichopo katika bajeti kwa ajili ya uendelezaji wa Stendi ya Laela ni shilingi 34,000,000/= tu (Mapato ya Ndani) na kuwa na upungufu wa shilingi 42,497,000/=, kiasi hiki cha fedha kinaombwa ili kunusuru Stendi hiyo iweze kufanya kazi wakati wote.

**3. Upanuzi wa eneo la stendi na kuanzisha eneo la kuegeshea malori**

Katika suala hili ilielezwa kuwa, ili kuchochea na kuharakisha ujenzi wa vibanda, inashauriwa itolewe fidia ya eneo la kuegeshea malori ili kazi hii ianze mara moja. Kufunguliwa kwa eneo la kuengesha malori kutakuza biashara katika eneo hilo hivyo kuchochea kuongezeka kwa kasi ya ujenzi wa vibanda vya biashara.

Iwapo utekelezaji utafanyika kwa wakati, una athari chanya ya kuchochea kasi zaidi ya ujenzi wa vibanda vya stendi kazi ambayo kwa sasa inasuasua. Lakini hali hiyo itafanya eneo hilo kuchangamka na kukua kibiashara na hatimaye Halmashauri kuongeza ukusanyaji wa mapato. Pia Maamuzi hayo ni mkakati kwa ajili ya kuongeza mapato ya ndani, kupanua mji wa Laela, kupanga mji wa Laela, kupunguza migogoro ya ardhi hapo baadaye kati ya serikali na Wananchi na pia uongozi wa sasa utaacha alama kubwa kwa kutenga eneo hilo kwa matumizi hayo.

Hivyo, kutokana na hali hiyo Kamati inashauri kuwa kiasi kilichotengwa cha shilingi 20,000,000 kwa ajili ya fidia wa eneo hilo, kianze kutumika kulipa fidia kwa wamiliki wa ardhi wa maeneo hayo kabla ya msimu wa kilimo haujafika ili kuwazuia wasilime na kuendeleza shughuli nyingine. Pia kwa kuwa Halmashauri inatarajia kuuza viwanja eneo la magharibi ya Kituo cha Polisi; Kamati inashauri mara baada ya mauzo fedha hizo zipelekwe kulipa fidia ya upanuzi wa stendi ya malori ili kukamilisha kutwaa eneo hilo na kuruhusu upimaji.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Wajumbe waliipokea na kuiridhia.

**...TASI NA. SDC/FAP-05/13/10/2021-2022: OMBI LA KUIDHINISHIWA MATUMIZI YA ...S 28,350,000/= KWA AJILI YA UKAMILISHAJI WA MIRADI YA MAENDELEO.**

Iliwasilishwa taarifa kuwa, kwa mwaka wa fedha, 2021/2022, Halmashauri inaomba kupeleka fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa miradi ya maendeleo ya Idara ya Afya, Elimu Msingi, na Sekondari ambayo inatekelezwa kwa kutumia Wananchi na miradi ya kimkakati ambayo ni ujenzi wa vyoo vya minada ya mifugo katika Kata ya Kilyamatundu na Muze pamoja na ukarabati wa Nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji Laela. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo;-

1. Ukarabati wa choo cha mnada wa mifugo Kilyamatundu - 2,000,000/=
2. Ukarabati wa choo cha mnada wa mifugo Muze - 3,000,000/=
3. Uendelezaji wa shule ya Sekondari Mnokola - 4,200,000/=
4. Uendelezaji wa shule shikizi na Ng'ongo - 2,000,000/=
5. Uendelezaji wa zahanati ya Kisa - 3,000,000/=
6. Ukarabati wa nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji Laela - 14,000,000/=

Baada ya kuwasilishwa taarifa hiyo, Wajumbe waliipokea na kuridhia mapendekezo hayo.

**MUHTASI NA. SDC/FAP-05/14/10/2021-2022: MAPENDEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI.**

Iliwasilishwa taarifa kuwa, Halmashauri imepokea fedha mbalimbali za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kiasi cha Shilingi 4,296,100,000/= ikiwa ni fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Hospitali, Vituo vya Afya, Madarasa na Vyoo, kama ifuatavyo;-

| N/S | JINA LA MRADI | FEDHA ILIYOTENGWA | FEDHA ZILIZOTOLEWA | AINA YA MRADI | MAPENDEKEZO YA MATUMIZI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Kituo cha Afya Tarafa ya Kipeta | 0 | 250,000,000/= | | 250,000,000 |
| 2 | Ujenzi wa kituo cha Afya Kaoze | 400,000,000/= | 100,000,000/= (fedha za mapato ya ndani) | Ujenzi wa kituo cha afya | 100,000,000/= |
| 4 | Fedha za UVIKO 19 | 0 | 1,740,000,000 | Mpui Sekondari - madarasa 6 | 120,000,000/= |
| | | | | Uchile Sekondari madarasa 5 | 100,000,000/= |
| | | | | Miangalua sekondari madarasa 5 | 100,000,000/= |
| | | | | Lusaka Sekondari madarasa 4 | 80,000,000/= |
| | | | | shule ya Sekondari Kwela Madarasa 6 | 120,000,000/= |
| | | | | shule ya Sekondari Mzindakaya madarasa 6 | 120,000,000/= |
| | | | | Shule ya sekondari Lula | 100,000,000/= |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Makuzani Sekondari madarasa 6 | 120,000,000/= |
| | | | | Ilemba Madarasa 6 | 120,000,000/= |
| | | | | Kaoze Sekondari madarasa 6 | 120,000,000/= |
| | | | | Kapenta sekondari 4 | 80,000,000/= |
| | | | | Kikwale shule ya msingi madarasa 4 | 80,000,000/= |
| | | | | Kipeta Sekondari madarasa 3 | 60,000,000/= |
| | | | | Mazoka Sekondari madarasa 6 | 120,000,000/= |
| | | | | Vuma Sekondari madarasa 7 | 140,000,000/= |
| | | | | Milenia sekondari 6 | 120,000,000/= |
| | | | | JUMLA NDOGO 1,740,000,000/= | |
| 5 | Fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyoo Matundu 48 katika Shule 7 za Msingi | 0 | 52,800,000 | Shule ya Msingi Laela B | 6,600,000/= |
| | | | | Shule ya Msingi Igonda | 6,600,000/= |
| | | | | Shule ya Misngi Mtowisa A | 6,600,000/= |
| | | | | Shule ya Msingi Sakalilo | 6,600,000/= |
| | | | | Shule ya Msingi Uzia | 6,600,000/= |
| | | | | Shule ya Msingi Tuwi | 6,600,000/= |
| | | | | Shule ya Msingi Nankanga | 6,600,000/= |
| 6 | Fedha kwa ajili ya ujenzi w nyumba za Waganga Hospitali ya Mtowisa | 0 | 90,000,000/= | Ujenzi wa nyumba tatu | 90,000,000 |
| 7 | Fedha kwa ajili ya ujenzi wa bweni la Wanafunzi wenye mahitaji maalum Shule ya Msingi Mkamanye | | 80,000,000/= | Ujenzi wa bweni | 80,000,000/= |
| 8 | Ujenzi wa Madarasa 17 katika Shule tano Shikizi | 0 | 340,000,000 | Shule ya Msingi Mwadui | 100,000,000/= |
| | | | | Shule ya Msingi Sofia Town | 40,000,000/= |
| | | | | Shule ya Msingi Kilando | 40,000,000/= |
| | | | | Shule ya Msingi Kikwale | 100,000,000/= |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Shule ya Msingi Namonka | 60,000,000/= |
| | | **JUMLA NDOGO 340,000,000/=** | | |
| [illegible] | Ujenzi wa vyoo Matundu 34 Shule ya Msingi Mpui A | | 43,300,000 | Ujenzi wa vyoo | 43,300,000 |
| 10 | Ujenzi wa Wodi 3 Hospitali ya Wilaya Mtowisa | 500,000,000 | 500,000,000 | | |
| 11 | Ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Laela | 1,000,000,000 | 1,000,000,000 | | |

Taarifa hiyo ilieleza zaidi kuwa, katika utekelezaji wa miradi hii, kwa kuzingatia hali halisi ya Upungufu wa Watumishi hususan katika Idara ya Ujenzi na Manunuzi ambazo hazina wakuu wa Idara wenye Sifa huku tukitambua umuhimu wao katika Utekelezaji wa Miradi ya maendeleo, Menejimenti ya Halmashauri itumie mfumo wa "single source" kwa kutumia taasisi za Serikali na baadhi ya Wakandarasi wachache wenye sifa katika Utekelezaji wa Miradi hiyo.

Taarifa hiyo ilieleleza zaidi kuwa utekelezaji huu unafuatia ushauri uliotolewa na ofisi ya RAS Rukwa kwa barua yenye Kumb.Na.CDC.109/232/03/37 ya tarehe 13 Septemba, 2021 ya kutumia mfumo huo kwa zingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa kuishirikisha bodi ya zabuni kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 kifungu Na.33.

Katika utekelezaji wa Ushauri huo, na kwa kuzingatia Jiografia ya Halmashauri yetu, menejimenti ya Halmashauri ilifanya tathimini na kutoa mapendekezo ya Mgawanyo wa Wakandarasi/Watoa huduma baada ya kufanya mashauriano na baadhi yao kama ifuatavyo:-

| N/S | MIRADI | KIASI CHA FEDHA | JUMLA | MAKANDARASI ANAYEPENDEKEZWA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Kituo cha Afya Kipeta | 250,000,000/= | 250,000,000/= | Jeshi la Magareza Rukwa |
| 2 | Ujenzi wa Kituo cha Afya Kaoze | 100,000,000/= | 100,000,000/= | Jeshi la Magereza Rukwa |
| 3 | Ujenzi wa vyoo shule ya Msingi Mpui | 42,300,000/= | 162,300,000/= | Mzabuni A |
| | Ujenzi wa madarasa 6 | 120,000,000/= | | |
| 4 | Ujenzi wa vyoo Shule ya Msingi Laela B | 6,600,000/= | 137,600,000 | Mzabuni B |
| | Uchile Sekondari madarasa 5 | 100,000,000/= | | |
| | Ujenzi wa vyoo shule ya Sekondari Uchile | 31,000,000/= | | |
| 5 | Miangalua sekondari madarasa 5 | 100,000,000/= | 100,000,000/= | Mzabuni C |
| 6 | Lusaka Sekondari madarasa 4 | 80,000,000/= | 200,000,000 | Mzabuni D |



CamScanner

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kwela Sekondari Madarasa 6 | 120,000,000/= | | |
| 7 | Mzindakaya Sekondari madarasa 6 | 120,000,000/= | 220,000,000/= | Mzabuni E |
| | Lula Sekondari Madarasa 5 | 100,000,000/= | | |
| 8 | Makuzani Sekondari Madarasa 3 | 60,000,000/= | 180,000,000/= | Mzabuni F |
| | Unyiha Sekondari Madarasa 6 | 120,000,000/= | | |
| 9 | Ilemba Madarasa 6 | 120,000,000/= | 870,000,000/= | Suma JKT |
| | Ujenzi wa Vyoo Shule ya Msingi Sakalilo | 6,500,000/= | | |
| | Kaoze Sekondari madarasa 6 | 120,000,000/= | | |
| | Ujenzi wa vyoo Shule ya Msingi Igonda | 6,600,000/= | | |
| | Kapenta sekondari 4 | 80,000,000/= | | |
| | Kikwale sekondari madarasa 4 | 80,000,000/= | | |
| | Kipeta Sekondari madarasa 3 | 60,000,000/= | | |
| | Mazoka Sekondari madarasa 6 | 120,000,000/= | | |
| | Ujenzi wa vyoo Shule ya Msingi Muze | 6,600,000/= | | |
| | Vuma Sekondari madarasa 7 | 140,000,000/= | | |
| | Shule ya Msingi Mtowisa A Ujenzi wa vyoo | 6,600,000/= | | |
| | Milenia sekondari | 120,000,000/= | | |

Baada ya kuwasilishwa taarifa hiyo wajumbe waliijadili na yafuatayo yalijitokeza.

**Suala la kuanza kutekekelezwa kwa mradi**

Wajumbe walieleza kuwa kutokana na gharama za utekelezaji wa miradi hii kama ilivyoanishwa katika BOQ, Wakandarasi wengi hawatakubali kufanya kazi hii na hivyo wajumbe waliridhia miradi hii kuanza kutekeleza kwa kutumia mfumo wa 'Force account' na Waheshimiwa Madiwani watatakiwa kusaidia kusimamia utekelezaji wa miradi hii ili iweze kukamilika kwa wakati.

Kwa upande wa matumizi ya nguvu za Wananchi, Wajumbe waliridhia kuwa nguvu za wananchi lazima zitumike katika utekelezaji wa miradi hii kwani fedha zilizotolewa hazitoshi kuwezesha kukamilisha mradi.



CamScanner

**MUHTASI NA. SDC/FAP-05/15/10/2021-2022: MPANGO KAZI NA REJISTA YA KAZI ZA KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.**

Uliwasilishwa mpango kazi na rejista ya Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ikionesha shughuli mbalimbali zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa kila robo mwaka ikiwa ni pamoja na;-

i. Kufanya ukaguzi katika Shule za Msingi na Sekondari kwa fedha za elimu bila malipo, P4R, SHWASH, LANES na TEA .
ii. Kufanya ukaguzi wa fedha za TASAF.
iii. Kufanya ukaguzi katika miradi ya maendeleo.
iv. Kufanya ukaguzi wa hesabu za mwisho kwa kipindi cha robo ya kwanza inayoishia Septemba 2021
v. Kufanya ukaguzi wa fedha za Mfuko wa Pamoja, Walter Reed, UVIKO - 19 na miradi mingine ya Afya.
vi. Kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi katika akaunti zote za Halmshauri.
vii. Kufanya ukaguzi wa mali za kudumu za Halmashauri.
viii. Kufanya ukaguzi wa manunuzi.
ix. Kufanya kaguzi maalum pale itakapoagizwa.
x. Kufanya majukumu mengine pale itakapoagizwa na mamlaka husika.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Wajumbe waliipitia na kuiridhia.

**MUHTASI NA. SDC/FAP-05/16/10/2021-2022: MAOMBI YA KUBADILI MATUMIZI YA FEDHA SHS 10,000,000/= KUTOKA CHANJO YA MIFUGO KWENDA UKARABATI WA MACHIJIO LAELA**

Iliwasilishwa taarifa kuwa kwa sasa machinjio ya Laela imeharibika kwa kiasi kikubwa, hasa sehemu ya kutolewa taka na maji machafu hali inayosababisha taka nyingi kutuama na kuwa sehemu ya mazalia makubwa na nzi.

Hivyo, ili kuweza kufanya ukarabati wa machinjio hiyo, Menejimenti ya Halmashauri inapendekeza fedha shs 10,000,000/= zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya chanjo ya mifugo dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu zipelekwe kufanya ukarabati wa machinjio ya mifugo Laela. Baada ya kuwasilishwa taarifa hiyo, Wajumbe waliipokea na kuridhia ombi hilo.

**MUHTASI NA. SDC/FAP-05/17/10/2021-2022: MAOMBI YA MKOPO WA FEDHA SHS 47,750,000/= KUTOKA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA AJILI YA MIRADI YA KUTWAA, KUPANGA, KUPIMA NA KUMILIKISHA ARDHI KATIKA MJI WA LAELA.**

Iliwasilishwa taarifa kuwa, Menejimenti ya Halmashauri inaomba idhini ya kukopa mkopo wa shs 47,750,000/= kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kutwa, kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika mji mdogo wa laela.



CamScanner

[illegible] hiyo itatumika kuandaa mchoro wa mipango mji, kufanya uthamini, kulipia fidia ekari [illegible] kapima.

Mwisho taarifa hiyo ilieleza fedha kiasi cha tshs 90,000,000/= kinatarajiwa kupatikana kutokana na mradi huo. Baada ya taarifa hiyo, kuwasilishwa wajumbe walipokea na kuiridhia.

## MUHTASI NA. SDC/FAP-05/18/10/2021-2022: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.

Hakukuwa na mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.

## MUHTASI NA. SDC/FAP-05/19/10/2021-2022: KUFUNGA KIKAO.

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufunga Kikao. Kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti wa kikao alieleza kuwa maagizo yote yaliyotolewa katika kikao hiki yafanyiwe kazi mara moja na pia alisisitiza suala la umaliziaji wa madarasa ya shule za Sekondari ili kuwezesha wanafunzi kuanza masomo ya kidato cha kwanza mapema mwezi Januari 2022.

Baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alifunga Kikao mnamo saa 11:20 jioni.

**UMETHIBITISHWA/HAUKUTHIBITISHWA**

KATIBU

Jina: Bi. Lightness Stanley Msemo

Sahihi: ............................

Tarehe: 02/12/2021

MWENYEKITI

Jina: Mhe. Kalolo Gerald Ntilla

Sahihi: ............................

Tarehe: 02/12/2021



CamScanner